

HALMASHAURI YA MJI HANDENI



SHULE YA SEKONDARI KOMNYANG'ANYO

KUMB.NA.KSS/S.2836/11

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

1.0 Kwa wanafunzi wote waliochaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Komnyang'anyo kwa mwaka 2021, wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.01 TAREHE YA KUFUNGUA SHULE

2.02 Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 mwanafunzi unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo mapema asubuhi saa 1:30 bila kukosa.

3.0 SARE ZA SHULE

3.01 Mwanafunzi anatakiwa awe na shati mbili (02) nyeupe mikono mifupi.

3.02 **WAVULANA** : Awe na suruali mbili, zishonwe marinda miwili (02) kushoto , na marinda mawili (02) kulia mifuko mitatu na luksi sita (06) suruali isiwe modo. Mkanda wa kuvalia suruali uwe mweusi

3.03 **Wasichana**: awe na sketi mbili(02) zishonwe kwa mtindo wa rinda box, rinda kubwa moja mbele na nyuma na marinda mawili ubavuni, sketi ndefu nchi mbili (02) au tatu (03) kuvuka magoti.

3.04 **VAZI LA HIJABU** au **SURUALI** vizingatiwe rangi ya sare ya shule mwanafunzi haruhusiwi kushona au kuvaa suruali inayo bana, Hivyo suruali iwe na upana wa kutosha.

3.05 Kitambaa cha sare ya shule kimeambatanishwa na fomu hii. Mzazi anahimizwa kuzingatia rangi sahihi ya kitambaa cha sare ya shule, endapo mwanafunzi atakuja tofauti na maelekezo ya fomu hii, sare hiyo haita kubaliwa.

3.06 Mwanafunzi (wavulana na wasichana) awe na viatu vya kawaida vya ngozi nyeusi vyenye kamba na kisigino kifupi na pia awe na raba za michezo.

4.0 VIFAA VYA DARASANI

4.01 Mwanafunzi awe na daftari 20, 10 za notsi na 10 za mazoezi, kalamu, penseli, rula na mkebe wa hesabu (Mathematical set) na begi jeusi la shule kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vya shule.

5.0 **CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI SHULENI.**

- Mwanafunzi alete nafaka/mahindi yaliyokobolewa kilo 25 kwa muhula
- Mwanafunzi alete maharage kilo 10 kwa muhula

6.0 **AFYA YA MWANAFUNZI**

6.1 Kwa mwanafunzi mwenye matatizo makubwa ya kiafya, mzazi afike shuleni kupata fomu ya Hospitali (MEDICAL CERTIFICATE FORM) kwa uhakiki na uthibitisho wa Daktari wa matatizo ya Afya ya mwanafunzi.

7.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu.

Angalizo:

Maendeleo ya taaluma na nidhamu yanategemea ushirikiano wa kina baina ya mzazi na walimu.

Karibu sana katika shule ya Sekondari Komnyang'anyo

.....

Martin I. Mwingo

Mkuu wa Shule

KOMNYANG'ANYO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by Medical Officer in respect for Form I/V Entrants

Pupil Name.....

Age.....

Blood cont (Red and White)
.....

Stool:.....

Urinalysis:.....

Syphili.....

T. B Test
.....

Ears:

Chest.....

Spleen:.....

Abdomen:.....

ADDITIONAL INFORMATION:

e.g Physical defects or impairments, infections. Chronic or family diseases etc.

.....
.....
.....

I certify the above is fit/ unfit for admission into a secondary school

Designation:

Station:

Date:

Official Stamp: